# MKATABA WA KUPANGA ENEO

**MKATABA HUU** umefanyika leo tarehe…01… mwezi……01…… mwaka…2021…….

Kati ya

ND ABDULRAHMAN M MUHIDIN
S.L.P 3810
DAR ES SALAAM

NA

…**ARK LOGISTICS LIMITED**..
……………………..

ORIGINAL

# MKATABA WA UPANGISHAJI

**MAKUBALIANO HAYA YAMEFANYIKA** siku ya tarehe ..01......ya mwezi wa..........01.........
.............mwaka **2021**

**BAINA YA**

Ndugu **Abdulrahman M Muhidin** wa sanduku la barua **3810**, ambaye ndani ya mkataba huu atakua anatajwa kama **MPANGISHAJI**

**NA**

Ndugu **.............. ARK LOGISTICS LTD.................** wa sanduku la barua ....**25109**..........., ambaye ndani ya mkataba huu atakua anatajwa kama **MPANGAJI**

**KWA KUWA:**

a) **MPANGISHAJI** ndiye, na ataendelea kuwa mmiliki halali wa eneo la cha biashara liliopo............**Pugu Road., Plot No 26/5 Industrial Area Ilala District Dar Es Salaam**...., Eneo ambalo ndani ya mkataba huu kinatajwa kama eneo la biashara

b) Na kwamba **MPANGISHAJI** ana hiaari, kwa kuzingatia kufuatwa kwa masharti yanayoainishwa kwenye mkataba huu, ya kumpangisha **MPANGAJI** eneo la biashara kwa ajili ya kufanyia biashara halali;

c) na kuwa **MPANGAJI**, kwa hiari yake, yuko tayari kupanga eneo hilo linacho pangishwa kwa kufuata, na bila kuvunja masharti yanayoainishwa katika mkataba huu;

**WAHUSIKA WA MKATABA HUU WANAKUBALIANA YAFUATAYO:**

a) **KWAMBA,** kwa malipo ya **KODI** inayoainishwa katika mkataba huu, na kulingana na masharti ya upangaji kama yanavyainishwa katika mkataba huu, **MPANGISHAJI** anaipangisha eneo la biashara kwa **MPANGAJI**;

b) **NA KWAMBA** mkataba huu utakua wa kipindi cha Miaka Mitano (5) Wenye Thamani ya Dola Za Kimarekani laki Moja (**100,000**) amabapo utaanza Siku ya tarehe**...01.....**mwezi wa **...01....**, mwaka ....**2021**........ mpaka Tarehe **31** mwezi **12**, mwaka **2025**

c) **NA KWAMBA MPANGAJI** atalipa Usd........**20,000**................. kwa mkupuo kwa **MPANGISHAJI**.

d)

ORIGINAL

e) **NA KWAMBA** mkataba huu umeanza kutumika Siku ya tarehe**...01.....**mwezi wa **...01....**, mwaka ....**2021**........ na utaisha tarehe **31** mwezi **12** mwaka **2025** ambapo **MPANGAJI** atarushusiwa kutumia eneo la biashara;

**KWA MASHARTI YAFUATAYO:**

a) Endapo

i katika kipindi cha upangaji kodi haitokua imelipwa kwa muda wa siku ishirini na moja na / au

ii **MPANGAJI**, bila sababu ya msingi, akashindwa kuzingatia masharti muhimu [1] ya upangishaji, katika mkataba huu; Itakua ni halali kwa mpangishaji, kutwaa chumba cha biashara;

b) Taarifa (NOTICE) inayohusiana upangaji katika mkataba huu itakua ni kwa njia ya maandishi;

c) Mkatabaa huu unaweza ukarefushwa kulingana na makubaliano wa wahusika wote wawili. Katika kipindi chote cha kupitia upya na kurefushwa kwake, kiasi cha kodi kitajadiliwa upya kulingana na mazingira ya kibiashara kwa wakati huo;

d) **MPANGAJI** anaweza akavunja mkataba kabla ya kumalizika kwa kipindi chake, baada ya kutoa taarifa kwa **MPANGISHAJI**: lakini kwa hali yoyota, uvunjaji wa mkataba ndani ya kifungu hiki hautoruhusu kurudishwa kwa **KODI** itakayokua imeshalipwa.

**KWA MASHARTI HAYO, MPANGAJI ANAKUBALI YAFUATAYO:**

1) Kulipa KODI kwa kwa kiasi kinachotajwa katika mkataba huu;
2) Kulipa Gharama za uafi, maji na umeme kwa mamlaka husika;
3) Kwa wakati wote, kuweka chumba cha biashara katika hali bora, na usafi kwa matumizi ya biashara;
4) Kuruhusu **MPANGISHAJI** au mtu yeyote kwa niaba yake, kuingia na kufanya matengenezo au ukaguzi unaohusiana na ubora wa chumba cha biashara;
5) Kutofanya upanuzi, au kubadilisha sehemu yoyote ya chumba cha biashara bila ridhaa ya **MPANGISHAJI;**
6) Kutompangisha mtu yoyote bila ridhaa ya **MPANGISHAJI;**
7) kutotumia chumba cha biashara kwa hali yoyote ambayo itasababisha kero au usumbufu kwa majirani au wafanyabiashara wengine;
8) Kutumia eneo la biashara kwa madhumuni ya biashara tu;
9) Kwamba Biashara itakayofanyika isiwe ni kinyume cha shsria za nchi;
10) Kwamba MPANGAJI atawajibika kwa uharibifu wa makusudi au uzembe, katika chumba cha biashara;

---

*[1] Masharti Muhimu ya upangishaji ni yale yanayo husiana na utunzaji wa chumba cha biashara, na malipo ya kodi.*

ORIGINAL

11) Wakati mkataba utakapofikia ukingoni, na kabla ya kurefushwa kwake, MPANGAJI atakabidhi chumba cha biashara kikiwa katika hali nzuri ya kibiashara.

**NA MPANGISHAJI ANAKUBALI YAFUATAYO:**

1) Kuhakikisha kwamba MPANGAJI hatopata usumbufu wowote, na kwamba baada ya MPANGAJI kulipa KODI na kutimiza masharti yote ya UPANGANI, MPANGISHAJI atakua huru kutumia chumba cha biashara kwa ajili ya madhumuni yanayoainishwa katika mkataba huu bila ya vikwazo vyovyote ambavyo ni kinyume na mkataba;
2) Kukifanyia matengenezo chumba cha biashara, na kuhakikisha kwamba wakati wote kiko katika hali nzuri kwa ajili ya biashara, pale ambapo hali itakayopelekea kuhitajika kwa matengenezo haitokuwa ni kwa ajili ya matendo ya **MPANGAJI**, kwa makusudi au uzembe, yatakayosababisha uharibifu;
3) Kulipa malipo yote katika mamlaka husika, malipo ambayo MPANGAJI hajatajwa kuhusika nayo katika mkataba huu.

MBELE YA MASHAHIDI, **MPANGAJI** amemlipa **MPANGISHAJI** kiasi cha Dola za Kimarekani ......2**0,000**......................... kama **KODI** kwa kipindi cha miezi .........**12**................; NA INASHUHUDIWA kwamba wahusika katika mkataba huu wameingia mkataba leo tarehe………**01/01/2021** na utaisha **tarehe 31** mwezi **12** mwaka **2025** kama inavyo onekana hapo chini:

**Jina na Sahihi ya MPANGAJI:**

Ndugu……ARK LOGISTIC LIMITED………………

Simu: ……………0784300303……………

Sahihi: ………………………………………………………

**Jina na Sahihi ya shahidi wa MPANGAJI:**

Ndugu……… …………………………

Simu: ……………………………………

Sahihi: ………………………………………………

**Jina na Sahihi ya MPANGISHAJI**

Ndugu…………… ABDULRAHMAN M KHAMIS ……

Simu: ……………………0784300303…

Sahihi: ………………………………………………

**Jina na Sahihi ya shahidi wa MPANGISHAJI**

Ndugu……………………………………………………

Simu: ………………………………………………

Sahihi: ………………………………………………